OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA
SHULE YA SEKONDARI PANKUMBI
MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA
KISWAHILI

021

MUDA SAA 2:30 **2018**

MAELEKEZO

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote.
3. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi uliyopewa.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu na mweusi.
5. Vifaa vyote vya mawasiliano haviruhusiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika namba yako ya mtihani katika kila kurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI		
NAMBA YA SWALI	**ALAMA**	**SAINI YA MTAHINI**
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
9		
10		
JUMLA		

SEHEMU A(ALAMA 15)

UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:
   " Kwa muda mrefu mashirika mengi ya umma yamekuwa yakikabiliwa na matatizo makubwa ya kifedha, wakati mwingine baadhi ya mashirika hayo huwa katika hatari ya kufilisika. Katika kujaribu kuyaokoa serikali mara nyingi imejaribu kuyapatia ruzuku au kuyaunganisha yale yenye shughuli zinazofanana.
   Katika mtiririko huohuo wa kujaribu kuyapatia uhai mashirika haya, serikali imeamua kuyapa uhuru zaidi, ambapo sasa yanaweza kupanga bei za huduma na bidhaa zao kwa lengo la kuyawezesha kujiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku.
   Tunatazamia kwamba mashirika yote yatatumia vizuri fursa hii ili kujiimarisha kiuchumi, na kwa kuzingatia ufanisi na kuepuka ubadhilifu na wizi wa mali na fedha ndipo vyombo hivi vitaweza kujikwamua kweli kweli.

Maswali:

i. Andika kichwa cha habari uliyoisoma kisichozidi maneno matano (5).
   ……

ii. Taja sababu tatu (3) zinazofanya mashirika ya umma kufilisika.
   ……
   ……
   ……

iii. Eleza jitihada zinazofanywa na serikali ili kuyaokoa mashirika ya umma yasifilisike. (Jitihada mbili (2))
   ……
   ……

iv. Eleza kwa kifupi maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika kwenye habari uliyoisoma.
   (a) Kujikwamua ……
   (b) Ruzuku ……
   (c) Kufilisika ……
   (d) Ufanisi ……
   (e) Ubadhilifu ……

v. Eleza ni kwanini wanawake ndio waletao mchango mkubwa wa maendeleo katika mataifa yao.
   ……

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiopungua 50 na yasiyozidi 60.

……
……
……
……
……
……

……
……
……
……

……
……

SEHEMU B (ALAMA 20)

SARUFI

3. (a) Nini maana ya mzizi wa neno?

   ……
   ……

   (b) Onesha mzizi wa maneno yafuatayo:

   (i) Sikukuta ……
   (ii) Hakukukumbuka……
   (iii) Sitakula ……

4. (a) Tunga sentensi zenye vipashio vifuatavyo huku ukionesha vipashio hivyo katika sentensi husika:

   (i) W + t + N ……
   (ii) N+V+T+N ……
   (iii) N+Ts+ T+ N ……
   (iv) N+T+U+T……
   (v) W+V+t+N+V……

   (b) Andika **KWELI** kama sentensi ni sahihi na **SI KWELI** kama sentensi si sahihi.

   (i) Kitenzi “chezea” ni cha asili ya kigeni……

   (ii) Sarufi ndio uti wa mgongo wa lugha……

   (iii) Viambishi “hu”, “me”, “ki” ni viambishi vya vinavyoonesha wakati……

   (iv) Viambishi awali hutokea baada ya mzizi wa kitenzi……

   (v) Mama anaelekea <u>kwa mzee shabani</u>……
   E

SEHEMU C (ALAMA 20)
MAWASILIANO NA UTUMATUMIZI YA LUGHA

5. (a) Silabi ni nini? ……

   ……

   (b) Bainisha silabi zilizomo katika maneno yafuatayo:

   (i) Walipoondoka……

(ii) Vitamkwa……

(iii) Tunajishughurisha……

(iv) Oa……

6. (a) Sentensi zifuatazo ni tata. Toa maana mbili kwa kila sentensi ili kuthibitisha utata huo.
   (i) Ashura ameondoka kazini.
   (a)……
   (b)……
   (ii) Tafadhari nipe sahani ya kulia.
   (a)……
   (b)……
   (iii) Baba john amefika.
   (a)……
   (b)……
   (iv) Ameiba kanga.
   (a)……
   (b)……
   (v) Wizi wa silaha umeongezeka.
   (a)……
   (b)……

   (b) Oanisha orodha A na orodha B ili kujenga dhana sahihi. Onesha majibu yako kwa kutumia kisanduku ulichopewa. Namba (i) umepewa kama mfano.

ORODHA A	**ORODHA B**
i. Dayalojia. ii. Misimu iii. Rejesta. iv. Konsonati. v. Kiimbo. vi. Fonimu. vii. Msamiati. viii. Lugha fasaha. ix. Mnyambuliko. x. Kidahizo.	(a) Ni lugha inayofuata taratibu zote za lugha kimaana, kimuundo na kimatamshi. (b) Neno lolote linaloingizwa kwenye kamusi ili lifafanuliwe kwa kupatiwa maelezo yanayohusu taarifa za kisarufi, kimaana na matumizi mbalimbali. (c) Kupanda na kushuka kwa sauti. (d) Mkazo katika neno. (e) Jumla ya maneno katika lugha. (f) Ni kitamkwa kidogo cha msingi chenye maana kisarufi. (g) Mtindo wa lugha unaotumika mahali fulani penye shughuli ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida. (h) Mfumo wa sauti za nasibu zenye kubeba maana zilizokubaliwa na watu zitumike katika mawasiliano. (i) Jumla ya maneno katika lugha yenye maana fulani (j) Namna ya kuunda neno jipya kwa kutumia neno la awali kwa kulirefusha neno. (k) B, ch, f, d, k, z. (l) Mazungumzo/majibizano ya kupokezana baina ya watu wawili au Zaidi.

	(m) Ubepari, ukweli na uwazi, hapa kazi tuna ngangari.

ORODHA A	i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x
ORODHA B										

SEHEMU D (Alama 30)

FASIHI KWA UJUMLA

7. "Fasihi simulizi ikihifadhiwa hudumu kwa muda mrefu". Taja njia tano za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi na kisha toa faida moja kwa kila njia

(i) Njia:……

Faida:……

(ii)Njia:……

Faida:……

(iii)Njia:……

Faida:……

(iv)Njia:……

Faida:……

(v)Njia:……

Faida:……

8. Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

(i) Visakale……

……

(ii) Maigizo……

……

(iii) Kitendawili……

……

(iv) Ngonjera

……

……

(v) Mandhari……

……

9. Soma ngonjera ifuatayo kisha jibu maswali:

A. La mgambo likilia, ujue kuna jambo,
Nimesimama kulia, umma uyaseme mambo,
Jamii inaugua, sasa twaenenda shombo,
Gonjwa hili gonjwa gani, mbona wengi walipenda?

B. Ndugu yangu mlimwengu, mbona wazidi lalama,
Kwani waona uchungu, hata kushika tama,
Gonjwa hili la kizungu, wengi wetu tutazama,
Nini hasa hamaniko, lako wewe mlimwengu?

C. Sikiliza ndugu, mdudu hatari kaingia,
Kupekecha kila mbegu, duniani kaingia,
Limekua kweli 'sugu', mauti kutuletea,
Gonjwa hili ni UKIMWI, hakika litakuua.

Maswali:

(i) Nini dhamira ya fanani katika utungo huu?
……
……

(ii) Umepata ujumbe gani kutoka kwenye ngonjera uliyoisoma?
……
……

(iii) Ni madhara gani jamii inayapata kutokana na ugonjwa huo unaozungumziwa kwenye ngojera? Taja madhara mawili (2)
……
……

(iv) Nini maana ya neno sugu? ……
……

(v) Taja sababu mbili zinazosababisha kutokea kwa ugonjwa huo:
(a) ……
(b) ……

SEHEMU E (Alama 15)

UANDISHI/UTUNGAJI

10. (a) Kadi ya mwaliko huundwa na vipengele mbalimbali. Taja vipengele vitano
(i) ……
(ii)……
(iiii)……
(iv)……
(v)……

(b) Andika kadi ya mwaliko wa harusi ya Wiliam Amani itakayofanyika tarehe 11.09.2018, katika kanisa la Mt. Joseph Mwanza na baadaye sherehe kwenye ukumbi wa SISIMIZI BAR Kirumba, kuanzia saa 1: 00 jioni.

.....
.....
.....

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA
MTIHANI WA MWISHO MWAKA -- 2018

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI
SOMO LA KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA

SEHEMU A (Alama 15)

UFAHAMU

1. Mtahiniwa anatakiwa asome habari kisha ajibu maswali aliyopewa kama ifuatavyo:
   (i) Abaini kichwa cha habari kisichozidi maneno matano (5)

   MASHIRIKA YA UMMA (Alama 1 $^{1}/_{2}$)

   nb: Aandike kichwa cha habari kwa herufi kubwa

   (ii) Ataje sababu tatu zinazofanya mshirika ya umma kufirisika ambazo ni:
   (a) Matizo ya kifedha (b) kutegemea ruzuku kutoka serikalini (c) Ubadhilifu/matumizi mabaya ya fedha

   (Alama $^{1}/_{2}$ @ = 1 $^{1}/_{2}$)

   (iii) Aeleze jitihadi mbili zinazo fanywa na serikali ilikuokoa mashirika ya umma yasifilisike ambazo ni:
   (a) Kuyapatia mashirika ya umma ruzuku (b) kuyaunganisha na yenye shughuli zinazofanana.

   (Alama 1 @ = 2)

   (iv) Aeleze kwa kifupi maana ya maneno yaliyopigiwa msitari kama ifuatavyo
   (a) Kujikwamua **ni kuondokana na matatizo au kutotegemea msaada.**
   (b) Kufilisika **ni ile hali ya mashirika ya umma kushindwa kuzalisha mali kiasi kwamba matumizi ya uzarishaji kuzidi mapato.**
   (c) Ruzuku **ni fedha zitolewazo serikalini kusaidia mashirika ya umma au taasisi za umma.**
   (d) Ubadhilifu **ni utumiaji mbaya wa mali za shirika, serikali, kampuni na n.k.**
   (e) Ufanisi **ni hali ya utendekaji wa kazi kwa ubora zaidi.**

   (Alama 1 @ = 05)

2. Mtahiniwa anatakiwa afupishe habari aliyoisoma kwa maneno yasiyopungua 50 na yasiyozidi 60 kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:
   (a) Afupishe habari kwa maneno yake mwenyewe.
   (b) Azingatie alama za uandishi.
   (c) Asipotoshe mantiki ya habari. (Alama 1 @ = 05)
   (d) Azingatie idadi ya maneno elekezi.
   (e) Azingatie lugha fasaha.

SEHEMU B (Alama 20)

SARUFI

3. (a) Mtahiniwa aeleze maana ya mzizi wa maneno kama ifutavyo:
   Mzizi **ni sehemu ya neno inayobaki baada kuondoa viambishi awali na viambishi tamati au ni umbo la msingi la neno ambalo haliwezi kuchanganuliwa tena sehemu nyingine ndogo bila kupoteza utambulisho wake. Mfano neno anacheza mzizi ni a+na+chez+a mzizi wa neno ni –chez— (alama 2)**

   (b) Mtahiniwa aoneshe mzizi wa kila neno alilopewa kama ifuatavyo:
   (i) –kut-- (ii) -- kumbuk—(iii) – l -- **(alama 1 @ = 3)**

4. (a) Mtahiniwa atunge sentensi kwa kutumia vipashio alivyopewa na kuonesha kipashio hicho kwa kila neno husika kama ifuatavyo:
   (i) Wewe ni Simba.
   W t N
   (ii) Mtoto mchafu anakula ugali
   N V T N
   (iii) John alikuwa anasoma kitabu
   N Ts T N
   (iv) Mama anaimba na kupika
   N T U T
   (v) Yule mrefu ndiye mwanafunzi hodari
   W V t N V
   Alama $^{1}/_{2}$ @ aina ya neno = 10

   (b) Mtahiniwa aandike **KWELI** katika sentensi sahihi na **SI KWELI** katika sentensi ambazo si sahihi kama ifuatavyo:
   (i) KWELI (ii) KWELI (iii) SI KWELI (iv) SI KWELI (v) KWELI **(Alama 1 @ = 05)**

SEHEMU C (Alama 20)

MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

5. (a) Silabi **ni sehemu ya neno inayotamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Au Nisehemu ya neno inayoundwa na konsonati na irabu au irabu peke yake na hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti**. **(Alama 01)**

   (b) Matahiniwa abainishe silabi alizopewa kama ifutavyo:
   (i) wa—li—po—o—ndo—ka.
   1 2 3 4 5 6
   (ii) vi—ta—m—kwa
   1 2 3 4

(iii) Tu—na—ji—shu—ghu—li--sha
1 2 3 4 5 6 7

(iv) O—a **(Alama 1 @ = 04)**
1 2

6. Mtahiniwa aondoe utata katika sentensi alizopewa kwa kutunga sentensi mbili
(i) (a) Ashura ameenda kazini
(b) Ashura ametoka kazini amerudi nyumbani.
(ii) (a) Tafadhari nipe sahani iliyopo mkono wa kulia
(b) Tafadhari nipe sahani kama chombo cha kuwekea chakula
(iii) (a) Baba yake John amerudi kutoka safari
(b) Baba, "John amefika"
(iv) (a) Ameiba nguo aina ya Kanga
(b) Ameiba ndege aina ya kanga.
(v) (a) Wizi wa kutumia silaha umeongezeka.
(b) Wizi wa kuiba silaha umeongezeka. **(Alama 2 @ = 10)**

(b) mtahiniwa aoanishe maneno kutoka orodha A na B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kama ifuatayo:

ORODHA A	i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x
ORODHA B	L	M	G	K	C	F	I	A	J	B

(Alama $^{1}/_{2}$ @ = 05)

SEHEMU D (Alama 30)

FASIHI KWA UJUMLA

7. Mtahiniwa ataje njia za uhifadhi wa fasihi simulizi na faida moja kwa kila njia kama ifuatavyo:
(i) Njia:Njia ya maandishi
Faida: Hudumu kwa muda mrefu
(ii)Njia: Kanda za kunasa sauti/ vinasa sauti.
Faida: msanii huweza kuwafikia watu walio mbali.
(iii) Njia: Njia ya kompyuta
Faida: Kazi za fasihi hutolewa pale unapohitajika.
(iv) Njia: Njia ya kanda za video
Faida: Wasanii pamoja na vifaa wanavyoytumia huonekana
(v) Njia: Njia ya kichwa
Faida: uwasilishaji hufanyika wakati wowote.
(alama 2 @ = 10, njia alama 1 na faida alama 1)
Tanibihi: Mtahiniwa akitaja njia zingine pamoja na faida tofauti na hizi apewe alama.

8. Mtahiniwa atoe maana ya istilahi alizopewa kama ifuatavyo:
(i) Visakale ni hadithi ambazo husimulia matukio ya kale
(ii) Maigizo ni masimulizi yanayoambatana na matendo kwenye jukwaa mbele ya hadhira

(iii) Kitendawili ni kipera ambacho hufanya kazi ya kumfikirisha msikilizaji pia ni kama chemsha bongo.
(iv) Ngonjera ni maigizo yenye kutumia mashairi ambayo huwa na pande mbili zinazopinzana.
(v) Mandhari ni mazingira au sehemu ambayo hadithi au masimulizi yanafanyika.

(ALAMA 2 @ = 10)

9. Mtahiniwa asome ngonjera na kasha ajibu maswali aliyopewa kama ifuatavyo:
(i) Matatizo ya ugonjwa wa UKIMWI.
(ii) Ili kuepukana matatizo ya ugonjwa wa UKIMWI jamii ipewe elimu ya kutosha.
(iii) (a) Kupoteza nguvu kazi (b) Kusababisha umaskini (c) vifo
(iv) Sugu ni ugumu wa kitu au kitu kilichokomaa, kutosikia dawa au maumivu.
(v) (a) Kujamiaana na mtu mwenye maambukizi ya UKIMWI bila kutumia kinga.
(b) Kuchangia vitu vyenye ncha kali na mtu mwenye maambukizi ya UKIMWI
(C) Kuongezwa damu yenye maambukizi ya UKIMWI

(ALAMA 2 @ = 10)

SEHEMU E (Alama 15)

UANDISHI/UTUNGAJI

10. (a) Mtahiniwa ataje mambo matano (5) ya kuzingatia katika uandishi wa kadi ya mwaliko kama ifuatavyo:
(i) Jina la mwandishi na anwani yake.
(ii) Jina la mwandikiwa au mwalikwa.
(iii) Lengo la mwalikaji kwa ufupi
(iv) Tarehe ya mwaliko.
(v) Mahali pa kukutunia.
(vi) Wakati wa kukutania.
(vii) Jibu lipelekwe kwa nani. (**Alama 1 @ = 05)**

(b) Mtahiniwa aandike kadi ya mwaliko kwa kufuata vipengele (a) hapo juu. **(Alama 10)**

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA
MTIHANI WA UTIMILIFU KIDATO CHA PILI -- 2018
SOMO LA KISWAHILI
JEDWALI LA UTAHINI

Na	MADA	STADI ZA KUPIMWA						Idadi ya maswali	Asilimia ya maswali kwa kila ujuzi
		Maarifa	Ufahamu	Matumizi	Uchambuzi	Uundaji	Tathimini		
1	Ufahamu		1			1		2	20
2	Sarufi	1					1	2	20
3	Mawasiliano na utumizi wa lugha		1		1			2	20
4	Fasihi	1		1			1	3	30
5	Uandishi/ Utungaji					1		1	10
Idadi ya maswali		2	2	1	1	2	2	10	
Asilimia ya maswali kwa kila ujuzi		20	20	20	10	10	20		100